**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**

**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ARDHI, MALIASILI NA UTALII**

# TAARIFA YA KAMATI KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA WIZARA YA MALIASILI NA UTALII KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027

*[Imetolewa chini ya Kanuni ya 121 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, za Mwaka, 2025]*

Ofisi ya Bunge,
S.L.P. 941,
**DODOMA.**

**15 Mei, 2026**

# YALIYOMO

*Ukurasa*


**YALIYOMO** ..... I
**KIELELEZO YA MAJEDWALI** ..... II
**SEHEMU YA KWANZA** ..... 1
**1.0 MAELEZO YA JUMLA** ..... 1
1.1 UTANGULIZI ..... 1
1.2 MSINGI WA UCHAMBUZI ..... 2
1.3 MAWANDA YA UCHAMBUZI WA TAARIFA ..... 2
**SEHEMU YA PILI** ..... 4
**2.0 MATOKEO YA UCHAMBUZI NA TATHMINI** ..... 4
**2.1 MAELEZO YA JUMLA** ..... 4
**2.2 UCHAMBUZI WA UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026** ..... 4
2.2.1 UZINGATIAJI WA MAONI NA USHAURI WA KAMATI ..... 5
2.2.2 UKAGUZI WA MIRADI YA MAENDELEO ILIYOTENGEWA FEDHA ..... 7
2.2.2.1 UFAFANUZI WA JUMLA ..... 7
2.2.2.2 YATOKANAYO NA UKAGUZI WA MIRADI ..... 10
2.2.3 HATUA ILIYOFIKIWA KATIKA UKUSANYAJI WA MADUHULI ..... 12
2.2.4 MWENENDO WA UPATIKANAJI WA FEDHA ZA MATUMIZI KUTOKA HAZINA ..... 14
2.3 UCHAMBUZI WA MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027 16
2.3.1 MAKADIRIO YA MAPATO KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027 ..... 16
2.3.2 MAKADIRIO YA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027 ..... 18
2.3.3 UCHAMBUZI WA MAMBO MAHSUSI KATIKA SEKTA YA MALIASILI NA UTALII. ..... 20
**SEHEMU YA TATU** ..... 31
**3.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI** ..... 31
3.1 MAONI YA JUMLA ..... 31
3.2 USHAURI WA KAMATI KATIKA MAENEO MAHSUSI KWA WIZARA YA MALIASILI NA UTALII ..... 31
3.3 HITIMISHO ..... 35

## KIELELEZO YA MAJEDWALI

**Kielelezo Na. 1:** Ukusanyaji wa Maduhuli hadi Februari, 2026 ........................................ 13

**Kielelezo Na. 2** Mwenendo wa Upatikanaji wa Fedha hadi Februari, 2026.............. 15

**Kielelezo Na. 3** Ulinganisho wa Makadirio Makusanyo ya Maduhuli kwa Mwaka wa Fedha/2026 na 2026/2027 .................................................... 17

**Kielelezo Na. 4** Ulinganisho wa Makadirio ya Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 na 2026/2027 ......................................................................... 19

**TAARIFA YA KAMATI KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA WIZARA YA MALIASILI NA UTALII KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027**

---

## SEHEMU YA KWANZA

## 1.0 MAELEZO YA JUMLA

### 1.1 Utangulizi

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 121 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge za Mwaka 2025, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii **(Fungu 69)** kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

**Mheshimiwa Spika,** ili kurahisisha mtiririko wa maudhui pamoja na kuzingatia masharti ya Kanuni ya 145 ya Kanuni za Bunge yanayohusu taarifa yoyote ya Kamati inayowasilishwa Bungeni, taarifa hii imegawanyika katika sehemu kuu tatu kama ifuatavyo: -

(i) Sehemu ya kwanza ni utangulizi inayotoa Msingi wa Uchambuzi na Mawanda ya Uchambuzi;

(ii) Sehemu ya pili inayotoa uchambuzi na tathmini ya Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026; pamoja na uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa Fedha 2026/2027; na

(iii) Sehemu ya tatu inayofafanua Maoni na Ushauri wa Kamati unaotolewa kwa Serikali pamoja na kuhitimisha taarifa ya uchambuzi wa bajeti.

### 1.2 Msingi wa Uchambuzi

**Mheshimiwa Spika**, Msingi wa Kamati wa kuchambua Taarifa ya Utekelezaji wa Majukumu na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maliasili na Utalii ni Masharti ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, ambapo Kanuni ya 6(8) (b) ikisomwa kwa pamoja na Kanuni ya 7(1)(a) zinatoa jukumu hilo kwa Kamati. Aidha, Kanuni ya 121(4) ya Kanuni za Bunge imeweka masharti yanayotaka Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kuchambuliwa na Kamati kabla ya kujadiliwa Bungeni.

**Mheshimiwa Spika,** ili kukidhi masharti hayo, Kamati ilipokea na kujadili Taarifa ya Wizara ya Maliasili na Utalii kuhusu Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027. Katika hatua hiyo, Kamati ilifanya uchambuzi wa kina na kuja na matokeo kama yalivyoainishwa katika taarifa hii.

### 1.3 Mawanda ya Uchambuzi wa Taarifa

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa ya Kamati inahusu utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii **(Fungu 69)** kwa mwaka wa Fedha 2025/2026 pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

**Mheshimiwa Spika**, Uchambuzi uliofanyika uligusa maeneo yafuatayo: -

(i) Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026;

(ii) Makadirio ya Mapato kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027;

(iii) Makadirio ya Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027; na

(iv) Mambo muhimu yanayogusa Sekta za Maliasili na Utalii.

**Mheshimiwa Spika,** wakati wa uchambuzi, Kamati iliongozwa na kigezo cha asilimia pamoja na kufanya tathmini ya jumla na ulinganisho wa mambo mbalimbali. Mambo hayo yaliwezesha Kamati kubaini hatua iliyofikiwa katika utekelezaji na mantiki ya mpango na makadirio kwa mwaka wa fedha unaokuja.

## SEHEMU YA PILI

## 2.0 MATOKEO YA UCHAMBUZI NA TATHMINI

### 2.1 MAELEZO YA JUMLA

**Mheshimiwa Spika,** Matokeo ya Uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti na Makadirio ya Mapato na Matumizi yanaweka msingi wa ushauri wa Kamati kuhusu hoja ya Waziri wa Maliasili na Utalii. Uchambuzi ulijielekeza katika maeneo mawili ambayo ni Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

### 2.2 Uchambuzi wa Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026

**Mheshimiwa Spika**, ili kuzingatia masharti ya Kanuni ya 120 (1) na (2) ya Kanuni za Bunge, Kamati ilichambua Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara hii baada ya ziara ya Ukaguzi wa Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha. Madhumuni ya sehemu hii ni kupata uelewa utakaolisaidia Bunge katika majadiliano yake kuhusu makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii. Aidha, sehemu hii inafafanua mambo manne yafuatayo: -

(i) Uzingatiaji wa Maoni na Ushauri uliotolewa na Kamati wakati wa kujadili Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026;

(ii) Hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo iliyoidhinishiwa fedha na Bunge;

(iii) Hali ya ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali; na

(iv) Mwenendo wa Upatikanaji wa Fedha za Matumizi kutoka Hazina.

**Mheshimiwa Spika,** mambo hayo kwa pamoja yameweka msingi wa kuliwezesha Bunge lako Tukufu kupata uwiano utakaolisaidia katika kufanya uamuzi baada ya mjadala wa Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maliasili na Utalii kama ilivyowasilishwa na mtoa hoja.

### 2.2.1 Uzingatiaji wa Maoni na Ushauri wa Kamati

**Mheshimiwa Spika,** katika kulisaidia Bunge kutekeleza jukumu lake la kuishauri Serikali, tarehe 19 Mei, 2025, wakati wa uwasilishwaji wa Hotuba ya Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Kamati ilitoa Maoni na Ushauri kuhusu mambo nane (08). Ili kupima tija ya Bunge kuendelea kuishauri Serikali, Kamati ilitaka kubaini iwapo ushauri uliotolewa umezingatiwa.

**Mheshimiwa Spika,** tarehe 26 Machi, 2026, Waziri wa Maliasili na Utalii alifika mbele ya Kamati kuwasilisha taarifa kuhusu hatua iliyofikiwa katika kuzingatia ushauri wa Kamati. Kamati ilichambua taarifa na kubaini kwamba, baadhi ya ushauri umezingatiwa na utekelezaji wake uko katika hatua mbalimbali. Kamati inaipongeza Wizara kwa hatua hiyo na kuendelea kusisitiza kuzingatia maoni na ushauri unaotolewa na Kamati na Waheshimiwa Wabunge katika kuboresha utekelezaji wa majukumu ya Wizara. Aidha, Kamati haikuridhishwa na utekelezaji wa maoni yafuatayo:-

(i) Pamoja na Serikali kuanza kutumia Mfumo wa kielektroniki (PAIS) katika ulipaji wa kifuta jasho na kifuta machozi kwa wananchi walioathirika na Wanyamapori wakali na waharibifu, bado Kamati inaona kasi ya ulipaji ni ndogo kulingana na mahitaji. Vilevile, kasi ndogo katika kuchukua hatua stahiki za muda mfupi, muda wa kati na muda mrefu katika kutafuta ufumbuzi wa changamoto zinazosababishwa na muingiliano baina ya binadamu na wanyamapori wakali na waharibifu kwa lengo la kunusuru maisha ya watu, wanyamapori na kuzuia uharibifu wa mali unaotokana na migongano hiyo;

(ii) Pamoja na maelezo ya Wizara kuhusu matumizi ya fedha za TDL, Kamati inaona bado malengo, mgawanyo, usimamizi na matumizi ya fedha hizo hauoneshi mwelekeo wa kuleta tija iliyokusudiwa kwa kuzingatia sababu au malengo hasa ya kurejeshwa kwa fedha hizi;

(iii) Serikali kushindwa kuchukua hatua za haraka kurudisha hoteli na loji toka kwa wamiliki waliobinafsishiwa hoteli na loji za Serikali ambao wamekiuka masharti ya mikataba ya kuziboresha na kuziendeleza; na

(iv) Serikali kushindwa kuiwezesha TTB kutekeleza majukumu yake kikamilifu kama chombo kilichopewa majukumu ya kutangaza na kuvutia utalii ndani na nje ya nchi.

**Mheshimiwa Spika,** uzingatiaji usioridhisha wa Maoni na Ushauri wa Kamati katika kutimiza majukumu ya Wizara, unaweza kupunguza ufanisi na kupelekea kuzorotesha ustawi wa wananchi

kinyume na lengo la Serikali katika Ibara ya 8 (1) (b) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

### 2.2.2 Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa Fedha

#### *2.2.2.*1 Ufafanuzi wa Jumla

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 120 (1) ya Kanuni za Bunge, Kamati ilifanya ziara katika mikoa mitatu **(3)** ya Manyara, Arusha na Kilimanjaro ili kukagua baadhi ya miradi inayotekelezwa na Wizara ya Maliasili na Utalii. Kamati ilikagua jumla ya miradi minne (04) ambayo ni: -

**(a) Mradi Na. 4314: Mradi wa Ujenzi wa Lango la Kuingilia katika Hifadhi ya Taifa Tarangire Eneo la Mamire**

**Mheshimiwa Spika,** mradi huu ulitekelezwa kwa thamani ya **Shilingi 3,921,704,476.60** ikiwa ni fedha zilizoidhinishwa na Bunge. Mradi ulipangwa kutekelezwa kwa kipindi cha miezi 28 kuanzia tarehe 10 Machi, 2023 hadi tarehe 30 Juni, 2025. Hata hivyo, wakati Kamati ilipotembelea mradi ilibaini kuwa, muda wa kukamilisha mradi umeongezeka hadi tarehe 14 Aprili, 2026.

**Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia tarehe 13 Machi, 2026, ambapo Kamati ilitembelea na kufanya ukaguzi wake, mradi ulikuwa umepokea **Shilingi 2,833,048,952.15** sawa na **asilimia 71.8** ya fedha zote za mradi.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilibaini kuwa, kutokana na changamoto ya upatikanaji wa fedha, mradi huu umeongezwa muda wa utekelezaji wake (*extension*) mara10. Ongezeko la muda wa utekelezaji linaweza kuambatana na

ongezeko la gharama kutokana na kupanda kwa gharama za mradi lakini pia kuchelewesha manufaa yaliyokusudiwa.

**(b) Mradi Na. 4814: Mradi wa Ujenzi wa Makumbusho ya Jiopaki (Geopark), Ngorongoro**

**Mheshimiwa Spika,** mradi huu ulitengewa **Shilingi Bilioni 32** kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya utalii na ujenzi wa makumbusho ya kisasa ya Jiopaki. Utekelezaji wa Mradi ulianza mwezi Juni, 2022 na ulitakiwa kutekelezwa ndani ya miezi 35 kuanzia Juni, 2022 hadi Mei, 2025.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilifanya ziara na kukagua mradi huo tarehe 13 Machi, 2026 na ilikuta mradi ukiwa umekamilika kwa **asilimia 100**.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Serikali kwa kukamilisha mradi huu wa makumbusho ya kisasa ambao kukamilika kwake kunatoa taswira halisi ya eneo la Hifadhi ya Ngorongoro pamoja na kuongeza uelewa kwa jamii juu ya thamani ya urithi wa jiolojia kwa kizazi cha sasa na vizazi vijavyo.

Kamati inaishauri Serikali kuendelea kuboresha mazingira ya eneo hili kwa kuweka vivutio vya aina mbalimbali kama vile maonesho ya tamaduni za makabila mbalimbali, maduka ya asili na maeneo ya huduma, hali itakayofanya watalii wavutiwe kukaa muda mrefu katika eneo hilo. Vilevile, Kamati inaishauri Serikali kuweka mikakati ya kutangaza makumbusho hii ili kuongeza watalii.

**(c) Mradi Na. 4812: Mradi wa Ujenzi wa Jengo la Mafunzo katika Chuo cha Usimamizi wa Wanyamapori, Mweka (CAWM)**

**Mheshimiwa Spika,** mradi huu umetokana na ongezeko la wanafunzi mwaka hadi mwaka katika chuo hiki uliopelekea chuo kutenga **Shilingi 3,799,982,716.9** kutoka vyanzo vya ndani kwa ajili ya ujenzi wa jengo jipya la mafunzo. Utekelezaji wa mradi huu ulianza tarehe 01Juni, 2022 hadi tarehe 31Mei, 2024.

**Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia tarehe 14 Machi, 2026 ambapo Kamati ilifanya ukaguzi wake, mradi ulikuwa umekamilika kwa **asilimia 100** na jengo limeanza kutumika rasmi mwaka wa masomo 2025/2026. Kukamilika kwa mradi huu kunatarajia kukiwezesha chuo kutoa mafunzo katika mazingira bora na yenye tija.

**(d) Mradi Na. 4313: Mradi wa Faru Weusi katika Hifadhi ya Taifa ya Mkomazi, Same**

**Mheshimiwa Spika,** mradi wa Faru Weusi katika Hifadhi ya Taifa ya Mkomazi Mkoani Kilimanjaro, umegawanyika kwenye miradi miwili ya kuzalisha Faru Weusi na Mbwambitu pamoja na Mradi wa Utalii wa Faru Weusi. Katika Mwaka wa Fedha 2025/2026, mradi ulitarajia kupanua uzio kwa kilomita za mraba 10 kwa lengo la kukabiliana na ongezeko la faru.

Hata hivyo, Kamati ilifahamishwa kuwa mradi huo haukutekelezwa kutokana na kupungua kwa fedha za miradi

za TANAPA kutoka **Shilingi Bilioni 144** hadi **Shilingi Bilioni 70.** Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha inatoa fedha za miradi kama zilivyoidhinishwa na Bunge ili kutekeleza miradi iliyokusudiwa na kwa wakati.

Vilevile, Serikali iweke mpango wa kutumia teknolojia ili kurahisisha upatikanaji wa faru (*tracking*) wakati wa utalii. Aidha, kwa kuzingatia ukubwa na ugumu wa kazi inayofanywa na wahifadhi wetu katika maeneo yote nchini, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha inaboresha maisha na maslahi yao kama sehemu ya motisha.

#### 2.2.2.2 Yatokanayo na Ukaguzi wa Miradi

**Mheshimwa Spika,** Katika ziara za ukaguzi wa miradi inayotekelezwa na Wizara ya Maliasili na Utalii, Kamati ilipokea taarifa za utekelezaji wa miradi na kuona hali halisi kwenye maeneo ya utekelezaji wa miradi husika. Lengo likiwa ni kulinganisha na kubaini iwapo taarifa zilizowasilishwa na Wizara zinawiana na hatua zilizofikiwa katika utekelezaji pamoja na madhumuni ya miradi inayohusika. Tathmini ya kina, imebainisha yafuatayo: -

(i) Kumekuwa na ucheleweshaji katika utekelezaji wa miradi mingi ya Wizara hali inayoweza kupelekea kuongezeka kwa gharama na kupunguza tija inayotokana na miradi husika;

(ii) Hali ya upatikanaji wa fedha za miradi kutoka hazina sio ya kuridhisha na Serikali inaweza kupata hasara ya kudaiwa riba na wakandarasi wanaotekeleza miradi hiyo. Mathalani katika utekelezaji wa Mradi Na. 4313 - Mradi wa Faru Weusi

katika Hifadhi ya Mkomazi, kulikuwa na mpango wa kupanua uzio kwa kilomita za mraba 10 ambao haukufanyika kutokana na kutopatikana kwa fedha. Mradi Na. 4313 wa ujenzi wa Lango la Mamire pamoja na miundombinu yake katika Hifadhi ya Tarangire, umechukua muda mrefu kukamilika kutokana na upatikanaji hafifu wa fedha za utekelezaji; na

(iii) Uwiano wa thamani ya fedha na miradi; Katika eneo hili, Kamati ilibaini uwepo wa uwiano wa thamani ya fedha na miradi kwa baadhi ya miradi lakini kwa upande mwingine uwiano wa thamani ya fedha na miradi ulikosekana. Kamati inaipongeza timu ya usimamizi ya Mradi Na. 4814: Ujenzi wa Makumbusho ya Jeopaki ya Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro ambapo utekelezaji wake na thamani ya fedha vinaonekana wazi ukilinganisha na miradi mingine ambayo Kamati ilikagua. Kwa mfano, Mradi Na. 4313 - Ujenzi wa Lango la Mamire na miundombinu yake katika Hifadhi ya Tarangire, ulikosa uwiano wa thamani ya fedha na mradi. Kamati ilipotembelea mradi huu, ilifahamishwa kuwa utekelezaji wake umefikia **asilimia 98.** Kamati haikuridhishwa na hali ya Mradi kwani ulionekana dhahiri una upungufu; kwa mfano, choo chenye matundu saba (7) kilichojengwa kwa **shilingi milioni 107**; Kamati inaona hakina thamani hiyo na lango lenyewe haliakisi thamani halisi. Mradi huu pamoja na kuwa ulitumia fedha nyingi, lakini pia uliongezewa muda wa utekelezaji wake. Jambo hili linaweza kuambatana na

ongezeko la gharama za ziada kutokana na kupanda kwa gharama za mradi.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na mambo hayo mahsusi yaliyobainika, Kamati pia ilibaini kuwa hali ya miundombinu ya barabara katika Hifadhi za Taifa sio ya kuridhisha, hali inayosababisha vivutio vingi kushindwa kufikika hasa nyakati za mvua. Mfano halisi ni Hifadhi ya Taifa ya Serengeti ambayo miundombinu yake kwa kiasi kikubwa iliharibiwa na mvua kiasi cha Kamati kushindwa kwenda kukagua Mradi wa Ujenzi wa Uwanja wa Gofu katika eneo la Fort IKoma; na barabara kutoka Babati kuelekea Lango la Mamire na sehemu ya kutoka Lango la Mamire kuingia Hifadhini.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaishauri Serikali kuandaa mpango mkakati wa kuhakikisha maeneo yote korofi katika miundombinu ya hifadhi yanapatiwa ufumbuzi wa kudumu ili yapitike nyakati zote. Sekta hii ya Utalii ambayo inachangia asilimia 17 ya pato la Taifa inapaswa kupewa kipaumbele katika kuhakikisha inapata mahitaji muhimu ya kuiwezesha kuendelea kuongeza tija.

### 2.2.3 Hatua iliyofikiwa katika Ukusanyaji wa Maduhuli

**Mheshimiwa Spika**, Lengo la uchambuzi wa taarifa za makusanyo ya maduhuli ni kuliwezesha Bunge kubaini iwapo lengo la makusanyo lililoidhinishwa na Bunge limefikiwa, lakini pia kutumia uzoefu unaopatikana kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 na kubaini uhalisia unavyostahili kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

**Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2025/2026, Wizara ilipangiwa kukusanya **Shilingi 1,185,584,115,330.55**. Hadi kufikia Februari, 2026, Wizara ilikuwa imekusanya **Shilingi 895,818,665,714.85** sawa na **asilimia 75** ya lengo la makusanyo lililokusudiwa. Kiwango hicho kinaashiria mwenendo mzuri wa ukusanyaji wa maduhuli.

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Kamati katika eneo la ukusanyaji wa maduhuli ulionesha kuwa ukusanyaji wa kutumia MNRT portal, umefikia **asilimia 65** ya lengo, huku ukusanyaji wa kutumia TRA umefikia **asilimia 79** ya lengo. Kupitia takwimu hizi, Kamati imewianisha muda wa utekelezaji wa bajeti na hatua iliyofikiwa katika ukusanyaji wa maduhuli na kubaini kuwa mwenendo huu wa makusanyo unaonesha kuwa lengo linaweza kufikiwa ifikapo mwisho wa mwaka wa fedha. Taswira kamili ya hali ya ukusanyaji inaonekana katika **Kielelezo Na. 1.**

**Kielelezo Na. 1: Ukusanyaji wa Maduhuli hadi Februari, 2026**

| Fungu 69 | % ya Makadirio | Makadirio (A) | Makusanyo (B) | Ufanisi (lengo vs makusanyo) |
|---|---|---|---|---|
| *MNRT Portal* | **27.45** | **325,478,017,370.65** | **216,203,800,995.54** | **66.42** |
| TRA (TANAPA& NCAA) | **72.55** | **860,106,097,959.74** | **679,614,864,719.31** | **79** |
| **JUMLA** | **100** | **1,185,584,115,330.55** | **895,818,665,714.85** | **75.56** |

***Chanzo:*** *Randama ya Wizara ya mwaka 2026 na usanifu wa Kamati*

**Mheshimiwa Spika,** kwa mchanganuo huo ni dhahiri kuwa, Makusanyo ya Taasisi za TANAPA na NCAA ndio yaliyofanikisha kwa kiasi kikubwa makusanyo kufikia **asilimia 75.56**. Kamati inaipongeza Wizara kwa hatua ya makusanyo iliyofikiwa. Vilevile, Kamati inaishauri Wizara kuongeza mikakati ya usimamizi katika kukusanya mapato kwa Taasisi zinazotumia mfumo wa MNRT Portal ili kuongeza tija katika ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali.

### 2.2.4 Mwenendo wa Upatikanaji wa Fedha za Matumizi kutoka Hazina

**Mheshimiwa Spika,** utekelezaji wa Bajeti unategemea upatikanaji wa fedha zilizoidhinishwa na Bunge. Kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Wizara iliidhinishiwa kutumia **Shilingi 336,518,895,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 254,232,349,000** sawa na **asilimia 75.5** zilikuwa fedha za Mtumizi ya Kawaida na **Shilingi 82,286,546,000** sawa na **asilimia 24.45** zilikuwa fedha za Miradi ya Maendeleo.

Hadi kufikia Februari, 2026, Wizara ilikuwa imepokea **Shilingi 206,903,257,247.13** sawa na **asilimia 62** tu ya fedha iliyoidhinishwa. Kati ya fedha hizo, **shilingi 163,517,161,157.05** sawa na **asilimia 64.32** zilikuwa za matumizi ya kawaida na **Shilingi 43,386,096,090.08** sawa na **asilimia 53** zilikuwa fedha za kugharamia Miradi ya Maendeleo. Taswira ya Upatikanaji wa Fedha inaonekana katika

**Kielelezo Na. 2.**

**Kielelezo Na. 2 Mwenendo wa Upatikanaji wa Fedha hadi Februari, 2026**

| Matumizi | | Kilichoidhinishwa | Kilichopokelewa | Asilimia |
|---|---|---|---|---|
| Kawaida | OC | 123,523,295,000 | 79,714,304,562.27 | 63.82 |
| | Mishahara | 130,709,054,000 | 83,775,856,594.78 | 51 |
| | **Jumla (A)** | **254,232,349,000** | **163,490,161,157** | **64** |
| | | | | |
| Maendeleo | Ndani | 32,476,051,000 | 8,521,937,479.36 | 26 |
| | Nje | 49,810,495,000 | 34,864,158,610.72 | 70 |
| | **Jumla (B)** | **82,286,546,000** | **43,386,096,090** | **53** |
| **JUMLA KUU (A+B)** | | **336,518,895,000** | **206,903,257,247.13** | **61.5** |

***Chanzo:*** *Randama ya Wizara 2026 na Usanifu wa Kamati*

**Mheshimiwa Spika,** ili kubaini kiwango cha utekelezaji wa bajeti, Kamati ilifanya uchambuzi kwa kuzingatia mwenendo wa upatikanaji wa fedha kutoka hazina ambapo unaonyesha kwamba hadi kufikia mwezi Februari, 2026: -

(i) Upatikanaji halisi ulitakiwa kuwa usiopungua **asilimia 66.67** ya Bajeti yote iliyoidhinishwa ili kuendana na muda wa utekelezaji wa bajeti, lakini Wizara ilikuwa imepokea **asilimia 61.5** tu. Hali hii inaweza kuchangia kushuka kwa ufanisi katika kutekeleza majukumu ya Wizara; na

(ii) Katika **asilimia 53** ya bajeti iliyopokelewa kwa ajili ya kugharamia utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo, fedha za ndani ni **asilimia 26** tu, huku fedha za nje zikiwa ni **asilimia 70** ya bajeti iliyoidhinishwa. Mwenendo huu wa upatikanaji wa fedha za ndani za maendeleo sio wa kuridhisha. Hali hii inaweza kupelekea miradi mbalimbali ya maendeleo na wakandarasi kushindwa kuendelea na kazi.

**Mheshimiwa Spika,** hali isiyoridhisha ya upokeaji wa fedha kutoka hazina kwenye utekelezaji wa shughuli za Wizara, ni moja ya kikwazo kikubwa katika kuhakikisha Wizara na Taasisi zake zinaendelea kukuza Sekta ya Utalii.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha inatoa fedha kama zilivyoidhinishwa na Bunge kwa kuwa ukamilishaji wa Miradi ya Maendeleo unaweza kuleta tija kama Serikali itazingatia utoaji wa fedha za kutosha na kwa wakati kama ilivyotarajiwa.

## 2.3 Uchambuzi wa Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilichambua na kujadili Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027. Uchambuzi wa Kamati ulijielekeza katika maeneo yafuatayo: -

(i) Makadirio ya Mapato kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027;
(ii) Makadirio ya Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2026/2026;
(iii) Ulinganisho wa Bajeti ya Wizara dhidi ya Bajeti ya Taifa; na
(iv) Mambo muhimu yanayogusa Sekta ya Maliasili na Utalii.

### 2.3.1 Makadirio ya Mapato kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027

**Mheshimiwa Spika,** kwa kutambua uhusiano uliopo kati ya Mapato na Matumizi, Kamati ilipokea ufafanuzi kuhusu lengo la maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 ambapo Wizara ya Maliasili na Utalii **(Fungu 69)** inakadiriwa kukusanya maduhuli ya **Shilingi 1,468,724,740,725.84.** Aidha, Kamati ilifanya uchambuzi kwa kuzingatia uzoefu uliopatikana katika ukusanyaji wa maduhuli kwa

Mwaka wa Fedha 2025/2026. Taswira ya ulinganisho wa makusanyo ya maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 na 2026/2027 inaonekana katika **Kielelezo Na. 3.**

**Kielelezo Na. 3 Ulinganisho wa Makadirio Makusanyo ya Maduhuli kwa Mwaka wa Fedha/2026 na 2026/2027**

| Fungu 69 | 2025/2026 | 2026/2027 | % ongezeko |
|---|---|---|---|
| Maduhuli yanayokwenda Mfuko Mkuu wa Serikali | 113,536,198,276.65 | 139,927,689,307.10 | 23.26 |
| Maduhuli yanayokusanywa na kutumika na taasisi | 1,070,047,917,053.90 | 1,328,797,051,418.74 | 24.18 |
| **JUMLA** | **1,183,584,115,330.55** | **1,468,724,740,725.84** | **24** |

***Chanzo***: *Randama ya Wizara 2026 na Usanifu wa Kamati*

**Mheshimiwa Spika,** Uchambuzi wa Kamati umebaini yafuatayo: -

(i) Makadirio ya ukusanyaji wa maduhuli yameongezeka kwa **Shilingi 214,742,096,850.55** sawa na **asilimia 24** ikilinganishwa na makadirio ya Mwaka wa Fedha 2025/2026. Aidha, kwa mtiririko wa makusanyo kwa mwaka unaoisha, unaonesha kuwa lengo la ukusanyaji wa maduhuli linaweza kufikiwa;

(ii) Makadirio ya Makusanyo ya maduhuli yanayokwenda Mfuko Mkuu wa Serikali yameongezeka kwa **asilimia 23.26** ikilinganishwa na Mwaka wa Fedha 2025/2026. Hata hivyo, ili kufikia lengo hili, Wizara iimarishe usimamizi wa mikataba ya uwekezaji katika maeneo yanayosimamiwa na TAWA pamoja

na usimamizi wa shughuli za kitalii ili kuongeza ufanisi katika ukusanyaji wa maduhuli;

(iii) Makusanyo ya maduhuli yanayokusanywa na kutumika na taasisi yameongezeka kwa **asilimia 24.18** ikilinganishwa na Mwaka wa Fedha 2025/2026. Ongezeko hilo limetokana na uamuzi wa Serikali kuruhusu baadhi ya taasisi kubaki na makusanyo yake ili kuongeza ufanisi katika kujiendesha; na

(iv) Katika lengo la Makusanyo ya Wizara, **asilimia 90.47** ya makusanyo, yatakusanywa na kutumika na taasisi zilizo chini ya Wizara ya Maliasili na Utalii, huku **asilimia 9.53** ya makadirio yatakusanywa na kupelekwa Mfuko Mkuu wa Serikali. Hali hii inaonesha dhamira ya dhati ya Serikali ya kuhakikisha Wizara na Taasisi zake hazikwami katika kutekeleza majukumu yake.

### 2.3.2 Makadirio ya Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027

**Mheshimiwa Spika,** ili kutekeleza mpango na vipaumbele vilivyowekwa katika Mwaka wa Fedha 2026/2027, Wizara ya Maliasili na Utalii **(Fungu 69)** inakadiria kutumia **Shilingi 334,345,870,000** kulinganisha na Makadirio ya Matumizi ya **Shilingi 336,518,895,000** katika Mwaka wa Fedha 2025/2026. Aidha, masharti ya Kanuni ya 120(2) ya Kanuni za Bunge yamelenga kuliwezesha Bunge kutumia uzoefu wa utekelezaji wa Bajeti kwa mwaka wa fedha unaoisha ili kuchambua makadirio ya matumizi kwa mwaka wa fedha unaofuata. Kwa kuzingatia lengo hilo, Kamati imechambua Makadirio ya Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 kwa kulinganisha makadirio hayo kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026. Taswira ya ulinganisho wa Makadirio ya Matumizi

kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 na 2026/2027 inaonekana katika **Kielelezo Na. 4.**

**Kielelezo Na. 4 Ulinganisho wa Makadirio ya Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 na 2026/2027**

| Mwaka | Matumizi ya Kawaida | | Maendeleo | |
|---|---|---|---|---|
| | PE | OC | Ndani | Nje |
| 2025/26 | 130,709,054,000 | 123,523,295,000 | 32,476,051,000 | 49,810,495,000 |
| 2026/27 | 144,691,490,000 | 127,352,935,000 | 23,134,770,000 | 39,166,675,000 |
| Pungufu/ongezeko | 13,982,436,000 | 3,829,640,000 | (9,341,281,000) | (10,643,820,000) |
| Asilimia % | 10.7 | 3.14 | -28.82 | -21.38 |

***Chanzo**: Randama ya Wizara 2026 na Usanifu wa Kamati*

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Kamati umeonesha kuwa:-

(i) Fedha za mishahara zimeongezeka kwa **Shilingi 13,982,436,000** sawa na **asilimia 10.7** ilinganishwa na Mwaka wa Fedha 2025/2026;

(ii) Fedha za Matumizi Mengineyo yaani (OC) zimeongezeka kwa **Shilingi 3,829,640,000** sawa na **asilimia 3.14** ikilinganishwa na Mwaka wa Fedha 2024/2025; na

(iii) Fedha za Miradi ya Maendeleo zimepungua kwa **Shilingi 19,985,101,000** sawa na **asilimia 24** ikilinganishwa na Mwaka wa Fedha 2025/2026. Aidha, fedha za ndani kwa Miradi ya Maendeleo zimepungua kwa **asilimia 28.82** huku fedha za nje zikipungua kwa **asilimia 21.38**.

**Mheshimiwa Spika**, upungufu wa **asilimia 24** wa fedha za Miradi ya Maendeleo unaweza kusababisha utekelezaji wa miradi kupunguza ufanisi na hivyo kupoteza tija iliyokusudiwa.

### 2.3.3 Uchambuzi wa Mambo Mahsusi katika Sekta ya Maliasili na Utalii

(i) **Changamoto ya Wanyamapori wakali na Waharibifu**

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na mafanikio yanayopatikana katika Sekta ya Maliasili na Utalii, migongano baina ya binadamu na wanyamapori ni moja ya **changamoto kubwa** inayoikabili sekta hii kwa sasa. Katika halmashauri 184 nchini halmashauri 91 sawa na **asilimia 49.5** zinakabiliwa na changamoto hiyo. Wanyama wanaoleta changamoto hii kwa sehemu kubwa ni pamoja na tembo, mamba, viboko, nyumbu, ngedere na nyani huku taarifa zikionyesha kwamba asilimia 80 ya migongano hiyo inasababishwa na mnyama tembo. Madhara yanayotokana na changamoto hiyo ni pamoja na vifo, ulemavu wa muda na wakudumu unaosababishwa na wananchi kujeruhiwa, uharibifu wa mali za wananchi kama vile mazao, miundombinu ya makazi, maji na barabara.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilifahamishwa kuwa sababu za migongano baina ya binadamu na wanyamapori ni kukosekana au kutozingatiwa kwa mipango ya matumizi bora ya ardhi, mabadiliko ya tabia ya nchi na ongezeko la mimea vamizi katika maeneo yaliyohifadhiwa, na kamati ilifahamishwa jitihada za Serikali za kupambana na changamoto hii ambazo ni kuongeza doria za udhibiti wa wanyamapori, ununuzi wa pikipiki za doria, ujenzi wa vizimba, uchimbaji wa visima na mabwawa katika maeneo ya hifadhi, ujenzi wa vituo vya askari, ufungaji wa visukuma mawimbi

kwa wanyamapori ambao ni viongozi wa makundi ya wanyama, uvunaji wa Wanyama mbalimbali ikiwemo tembo 100, kiboko 197, fisi 171 na mamba 153. Kielelezo kifuatacho kinaonesha utekelezaji wa mipango na jitihada za serikali kwa mwaka wa fedha 2025/2026.

**Kielelezo Na. 6: Utekelezaji wa Shughuli za kukabiliana na migongano baina ya Wanyamapori na Binadamu kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 hadi kufikia Februari, 2026**

| SHUGHULI ZILIZOTEKELEZWA HADI FEBRUARI, 2026 | | | |
|---|---|---|---|
| **SHUGHULI** | **MPANGO** | **UTEKELEZAJI** | **ASILIMIA YA UTEKELEZAJI** |
| **Ununuzi wa helikopta** | 02 | 0 | 0 |
| **Uchimbaji wa mabwawa** | 12 | 05 | 42 |
| **Ujenzi wa vizimba** | 50 | 45 | 90 |
| **Uchimbaji wa visima** | 18 | 10 | 56 |
| **Ujenzi wa uzio wa umeme** | Km. 53 | 0 | 0 |
| **Ujenzi wa vituo vya askari** | 19 | 20 | 105.3 |
| **Kuwajengea uwezo askari wa wanyamapori wa vijiji** | 100 | 410 | 410 |
| **Ununuzi wa pikipiki** | 22 | 33 | 150 |
| **Ununuzi wa ndege nyuki (drones)** | 12 | 0 | 0 |
| **Ununuzi wa mikanda maalum ya mawasiliano (Visukuma mawimbi)** | 50 | 52 | 104 |
| **Ununuzi wa mabomu baridi** | 40,000 | 0 | 0 |

**Chanzo:** *Randama ya Wizara ya Maliasili na Utali na Usanifu wa Kamati*

**Mheshimiwa Spika,** Pamoja na jitihada hizi za Serikali, kamati imebaini kwamba bado changamoto hii ni kubwa sana na athari, madhara na malalamiko yake ni Dhahiri. Hali hii inawaumiza wananchi, kuwakatisha tamaa na kuwachonganisha na Serikali yao.

**Mheshimiwa Spika,** Katika kupunguza maumivu ya changamoto hii kwa wananchi, Serikali iliweka utaratibu wa kutoa kifuta jasho na kifuta machozi kwa wananchi wanaokumbwa na changamoto hii. Hata hivyo, Kamati inaona bado kasi ya kutenga na kulipa fedha za kifuta jasho na kifuta machozi hairidhishi na hivyo wananchi wengi waliohakikiwa madai yao kutolipwa kwa wakati. Mathalani, hadi tarehe 21 Januari 2026 wizara ilikuwa imepokea madai kutoka kwa wananchi 62,446 yenye jumla ya **Shilingi Bilioni 18.67** kutoka katika Halmashauri 56 nchini, na hadi kufikia tarehe 20 Machi, 2026 wizara ilikuwa imelipa madai ya wananchi 15,153 tu yenye thamani ya **shilingi bilioni 7.2.** Bado wananchi 47,293 hawajalipwa madai ya **shilingi bilioni 11.47** na baadhi ya madai yamekuwepo kwa zaidi ya miaka miwili. Ucheleweshaji huu wa malipo unapoteza maana halisi ya kifuta jasho na kifuta machozi.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha inatenga na kutoa fedha ili kulipa madai kwa wakati; ifanye utafiti wa kina juu ya changamoto hii, na iendelee kuchukua hatua mbalimblai za utatuzi kama vile kujenga uzio wa umeme; kuchimba mabwawa kwenye maeneo ya hifadhi ili kupunguza tatizo la Wanyama kuhamahama kwenda kutafuta maji, kuongeza askari, vitendea kazi na kutoa elimu kwa wananchi.

(ii) **Hali ya Ujangili Nchini**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inatambua juhudi za Serikali za kupunguza/kupambana changamoto ya ujangili nchini ambapo katika miaka ya hivi karibuni imechukua hatua mbalimbali ikiwemo kutumia teknolojia ya mbwa maalum waliofunzwa kunusa nyara katika viwanja vya ndege na mipakani, matumizi ya teknolojia ya kisasa, kuboresha mafunzo, vitendea kazi kwa askari na kuongeza doria. Kupitia jitihada hizo, tumeshuhudia kuongezeka kwa idadi ya wanyamapori adimu kama vile faru. Hata hivyo, bado kuna changamoto ya biashara haramu ya nyara na uwindaji wa wanyama pori katika baadhi ya maeneo.

Kamati ilifahamishwa kuwa kupitia doria mbalimbali zaidi ya nyara 180 zilikamatwa, watuhumiwa wa ujangili 6,431 walikamatwa pamoja na silaha za aina mbalimbali 145 zilizotumika kufanyia ujangili.

**Mheshimiwa Spika**, Hali hii isipodhibitiwa inaweza kurudisha nyuma juhudi za Serikali ya Awamu ya Sita za kukomesha kabisa ujangili na kuinua utalii. Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha hali hii inadhibitiwa kabisa ili kuendelea kulinda rasilimali zetu kwa kuweka sheria kali; kuzisimamia; na kuwawezesha askari kwa kuwapa motisha zaidi ili waendelee kufanya kazi kwa bidii.

(iii) **Utalii wa Malikale**

**Mheshimiwa Spika,** utalii wa malikale nchini, unahusisha kutembelea maeneo ya kihistoria kama vile michoro ya mambo ya kale, magofu, mapango, mifupa ya Wanyama wa kale na makumbusho ili kujifunza utamaduni na historia. Tanzania imebarikiwa kuwa na maeneo mengi ya malikale ambayo Kamati inaona hayajawekewa mikakati ya kutosha ya kutangazwa ili kuvutia, kuongeza watalii wa ndani na nje pamoja na kukuza mapato yatokanayo na utalii.

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande mwingine, Kamati inaona kuna fursa ya kukuza utalii na kuongeza mapato ya Serikali kwa kuyapa kipaumbele maeneo ya kihistoria ambayo bado hayajatumika kikamilifu.

(iv) **Bodi ya Utalii Tanzania (*Tanzania Tourist Board-TTB*)**

**Mheshimiwa Spika,** Bodi ya Utalii Tanzania ni Taasisi ya Umma iliyoanzishwa kwa Sheria ya Bodi ya Utalii Tanzania Sura Na. 364 R.E 2002 ikitakiwa kuchukua majukumu ya lililokuwa Shirika la Utalii Tanzania (*Tanzania Tourist Corporation - TTC*). Sheria hiyo imeainisha majukumu ya TTB ambayo kimsingi ni kutangaza na kuendeleza aina zote za utalii nchini. Kifungu cha 5(1) cha Sheria ya Bodi ya Utalii Tanzania kinatamka wazi kuwa, moja ya kazi za Bodi ni: "*kuchukua hatua zote zinazostahili kutangaza na kuitangaza Tanzania kama kivutio maarufu cha utalii*" (*to adopt all*

*such measures as it may consider necessary to advertise and publicise Tanzania as a popular tourist destination*).

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imefanya uchambuzi wa taarifa mbalimbali zilizowasilishwa na Serikali kwa lengo la kupima ufanisi katika utendaji wa Bodi ya Utalii Tanzania. Katika uchambuzi wake, Kamati imebaini kuwa, pamoja na hatua za Serikali kuendelea na mchakato wa kufanya mapitio ya Sheria ya Uanzishaji wa Bodi hii ili kuihuisha iendane na mahitaji ya sasa, bado Bodi inakabiliwa na changamoto kubwa ya ufinyu wa bajeti katika kutekeleza majukumu yake. Vilevile, kuna muingiliano wa majukumu baina yake, Wizara na Taasisi nyingine ndani ya Wizara. Vilevile inakabiliwa na upungufu wa wataalam wa kutosha wenye uzoefu, ujuzi na ubobevu katika kutangaza utalii.

**Mheshimiwa Spika,** Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya 2025/2030 katika ukurasa wa 18 imeweka lengo la kuongeza mchango wa Sekta ya Utalii katika Pato la Taifa kutoka **asilimia 17** mwaka 2025 hadi **asilimia 20** mwaka 2030. Na moja ya mipango iliyojiwekea ni kuimarisha mikakati ya kutangaza na kuvutia watalii wa ndani na nje ya nchi kwa kuanzisha kampeni maalumu ya kufikisha idadi ya watalii milioni nane (8,000,000) kwa mwaka ifikapo mwaka 2030.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati haioni ni namna gani Bodi hii inaweza kuchangia kufikia malengo yaliyowekwa kwenye Ilani ya Uchaguzi ya kufikia watalii milioni 8

ifikapo 2030 ikiwa changamoto zilizoainishwa hazitapatiwa ufumbuzi wa haraka na wa kudumu. Kamati inaishauri Serikali kuweka mfumo utakaoiwezesha TTB kufanya shughuli zote za utangazaji utalii. Aidha, TTB iwezeshwe kufikia malengo yake ya kujitegemea ili kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi na kupunguza utegemezi wa fedha kutoka serikalini.

(v) **Hali ya Miundombinu katika vivutio vya Utalii Nchini**

**Mheshimiwa Spika**, Moja ya maeneo muhimu katika kufanikisha shughuli za utalii ni miundombinu ikiwemo barabara, madaraja na viwanja vya ndege. Kamati ilibaini kuwa hali ya miundombinu haswa barabara na madaraja katika baadhi ya maeneo ya vivutio vyetu sio ya kuridhisha na haikidhi mahitaji ya huduma na shughuli za Utalii na kufanya baadhi ya vivutio kutofikika au kufikika kwa shida hasa nyakati za mvua. Mfano, miundombinu katika Hifadhi ya Taifa ya Serengeti iliharibika kiasi cha kupunguza kasi ya utalii na kuleta taswira mbaya kipindi cha mvua na hali hii imekuwa ikijirudia mara kwa mara.

Kamati inaishauri Serikali kuweka mkakati mahsusi wa kuipatia changamoto hii ufumbuzi wa kudumu ili kuboresha mazingira ya utalii nchini.

(vi) **Tozo ya Maendeleo ya Utalii (TDL)**

**Mheshimiwa Spika,** katika kuendeleza sekta ya utalii nchini Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilianzisha Tozo ya Maendeleo ya Utalii (*Tourism*

*Development Levy - TDL*) mwaka 2013 kupitia Sheria ya Utalii, Sheria Na. 29 ya mwaka 2008 Kifungu cha 59(1) na 59(2) ambapo pia vyanzo vya mapato ya mfuko/tozo hiyo viliainishwa kuwa ni asilimia 3 ya mapato ghafi kutoka taasisi za Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA) na Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro (NCAA). Kutokana na mabadiliko ya Sheria ya Fedha ya mwaka 2020 yaliyosababisha mapato ya taasisi hizo za TANAPA na NCAA kukusanywa moja kwa moja na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), TDL ilisitishiwa kupokea fedha.

**Mheshimiwa Spika,** ili kutimiza azma yake ya kukuza na kuendeleza Sekta ya Utalii Nchini, Mheshimiwa Dkt Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, aliridhia kurejeshwa kwa Tozo ya Maendeleo ya Utalii nchini (TDL), ambayo ilikuwa imesitishwa. Bunge lako Tukufu lilifanya marekebisho kupitia Sheria ya Fedha ya mwaka 2024 ili kuruhusu **asilimia 6** ya mapato ghafi ya taasisi za TANAPA na NCAA kuwa chanzo cha tozo hiyo.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaendelea kumpongeza Mheshimiwa Rais, kwa uamuzi wake ambao unalenga kukuza sekta ya utalii nchini. Aidha, uamuzi wa kuidhinisha kiasi hicho cha fedha unaonesha nia ya dhati ya Bunge lako Tukufu katika kuunga mkono juhudi za Serikali kwenye kuleta maendeleo ya Sekta ya Utalii nchini.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini kuwa tangu kuanza kwa utekelezaji wa tozo hii, kumekuwa na changamoto kwenye vipaumbele, mgawanyo, utekelezaji na usimamizi wa shughuli zinazotekelezwa kwa tozo/fedha hizi. Kamati inaona mgawanyo na matumizi ya fedha hizi hautokani na hali, mahitaji halisi ya sekta wala mipango madhubuti ya kutangaza na kukuza utalii. Badala yake unagawanywa na kutumiwa kama fedha za dharura zilizokusanywa bila kuwepo kwa mahitaji.

Kamati inaishuri Serikali kutafakari upya malengo, mgawanyo na usimamizi wa fedha hizi ili tija iliyokusudiwa ipatikane.

(vii) **Migogoro ya Mipaka na Utwaaji Ardhi**

**Mheshimiwa Spika,** Migogoro ya mipaka na utwaaji wa ardhi katika maeneo ya uhifadhi nchini ni changamoto ya muda mrefu inayochochewa na ushindani wa matumizi ya ardhi kati ya shughuli za binadamu (kama kilimo na ufugaji) na malengo ya uhifadhi.

**Mheshimiwa Spika**, Migogoro mingi inatokana na kutokuwepo kwa alama za kudumu (vigingi) kati ya ardhi ya kijiji na maeneo ya hifadhi, jambo linalopelekea kuingiliana kwa shughuli za kiuchumi na uhifadhi haswa ikizingatiwa kuwa ongezeko la watu limesababisha ongezeko la uhitaji wa ardhi kwa ajili ya shughuli za kibinadamu. Pia kumekuwa na mazoezi ya utwaaji wa ardhi ya wananchi kwa ajili ya shughuli za uhifadhi

kwenye baadhi ya maeneo. Utwaaji huo umesababisha migogoro na malalamiko ya wananchi kucheleweshewa malipo ya fidia na/au kutoridhika na viwango vya fidia.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Serikali kwa kazi kubwa iliyofanywa na Kamati ya Mawaziri nane wa Kisekta iliyozunguka maeneo mengi nchini kutatua migogoro ya ardhi**.** Kamati inaishauri Serikali kuendelea kutatua migogoro ya mipaka kati ya maeneo yaliyohifadhiwa na wananchi ili kulinda amani, utulivu na uhifadhi wa rasilimali zetu. Aidha, Kamati inaitaka Serikali kuhakikisha inalipa fidia stahiki na kwa wakati inapotwaa maeneo kwa ajili ya uhifadhi kama Katiba na Sheria za Ardhi zinavyoelekeza.

(viii) **Mashindano ya Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON 2027)**

**Mheshimiwa Spika**, Uwepo wa Mashindano ya mpira wa miguu ya Kombe la Mataifa ya Afrika mwaka 2027 (AFCON 2027) ambayo Tanzania ni moja ya nchi wenyeji ni fursa ya kihistoria kwa Sekta za Uchumi na Utalii. Mashindano haya yanaweza kuwa kichocheo kikubwa kwa Sekta ya Utalii nchini ikiwa fursa hiyo itatumika kikamilifu kwa kuwa yanatarajiwa kutazamwa na kuleta maelfu ya mashabiki, wanahabari, wawekezaji na watalii kutoka Afrika na Duniani kote.

**Mheshimiwa Spika,** wakati Kamati ikichambua bajeti ya Wizara hii, haikuona mikakati mahsusi iliyowekwa na Wizara inayoonesha kushiriki na kutumia fursa ya uwepo wa mashindano haya kutangaza utalii. Kamati inaishauri Serikali kuweka mikakati madhubuti ili kutumia mashindano haya kuitangaza Tanzania na Vivutio vyake na kwa kuwafanya Wageni watakaokuja wakati wa mashindano haya kupata uelewa wa vivutio vyetu, waweze kuvitembelea na kuwa mabalozi wazuri wa Tanzania. Aidha, Serikali ihimize na kusimamia wamiliki wa hoteli kuziweka kwenye hadhi nzuri ili kuwezesha kupokea ugeni huu.

**SEHEMU YA TATU**

## 3.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

**Mheshimiwa Spika,** baada ya uchambuzi kuhusu Utekelezaji wa Bajeti pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maliasili na Utalii, sasa naomba kuwasilisha Maoni na Ushauri wa Kamati kama ifuatavyo: -

### 3.1 Maoni ya Jumla

(a) Serikali ihakikishe inaendelea kubuni mbinu mpya za kutangaza vivutio vya utalii ndani na nje ya nchi ili kuongeza idadi ya watalii wanaotembelea vivutio hivyo hali itakayochangia kuongeza mapato ya Serikali, kukuza uchumi na kuongeza ajira katika mnyororo wa thamani kwenye shughuli zitokanazo na utalii nchini; na

(b) Serikali iendelee kuibua na kuendeleza mazao ya utalii ya kimkakati, kuboresha miundombinu ya utalii na uhifadhi pamoja na kuimarisha matumizi ya teknolojia za kisasa katika usimamizi wa uhifadhi.

### 3.2 Ushauri wa Kamati katika Maeneo Mahsusi kwa Wizara ya Maliasili na Utalii

#### A. Hali ya Upatikanaji wa Fedha za Miradi ya Maendeleo

Kamati inashauri kuwa, Serikali:-

(i) Ihakikishe fedha za miradi zilizotengwa na kuidhinishwa na Bunge zinatolewa kwa wakati ili miradi iliyokusudiwa ikamilike kama ilivyopangwa lakini pia kuepuka kuzalisha gharama za ziada; na

(ii) Kupitia timu za usimamizi na ukaguzi wa miradi, ihakikishe thamani ya fedha katika miradi inayotekelezwa inaonekana.

**B. Changamoto ya Wanyamapori Wakali na Waharibifu**

Kamati inashauri kuwa, Serikali:-

(i) Ifanye utafiti wa kina wa sababu, athari na mbinu za kukabiliana na changamoto hii ili kupata suluhisho la kudumu.

(ii) Iandae na kuboresha Mkakati mpya wa Kitaifa wa kushughulika na mgongano kati ya binadamu na wanyamapori wakali na waharibifu ili kupata suluhisho la kudumu la changamoto hiyo kwa kushirikiana na wadau;

(iii) Iweke mpango mahsusi wa kulipa kwa wakati kifuta jasho na kifuta machozi kwa wananchi walioathiriwa na wanyamapori ili kuleta maana halisi ya kifuta jasho na kifuta machozi;

(iv) Iweke mkakati wa kuhakikisha kuwa, maeneo yote yenye changamoto kubwa ya muingiliano yanawekewa uzio wa umeme ili kuondokana na changamoto hii; na

(v) Ihakikishe inaendelea kuimarisha ulinzi katika hifadhi na mapori yetu ili kutokomeza ujangili.

**C. Utalii wa Malikale**

Kamati inashauri kuwa, Serikali iongeze na kuweka mikakati ya kuibua, kuanzisha na kutangaza utalii wa malikale.

**D. Changamoto ya Miundombinu ya Utalii**

Kamati inashauri kuwa, Serikali ihakikishe inaandaa mpango Madhubuti na mahususi wa Ujenzi na ukarabati wa miundombinu ili kupata ufumbuzi wa kudumu na kuwezesha maeneo ya vivuto vya utalii kufikika nyakati zote.

**E. Bodi ya Utalii Tanzania (TTB)**

Kamati inashauri kuwa, Serikali: -

(i) Iweke/iboreshe mfumo utakaoiwezesha TTB kufanya shughuli zote za utangazaji utalii bila kuingiliwa kama yalivyo madhumuni ya uanzishwaji wake;

(ii) Iongeze uwekezaji katika kutangaza utalii na fedha zinazotengwa zitolewe kwa wakati ili kufanikisha utangazaji wa kimkakati;

(iii) Iifanyie TTB mageuzi Makubwa ya kimuundo na kimajukumu ikiwa ni pamoja na kuipa wataalamu wenye ujuzi na ubobevu kwenye kutangaza utalii;

(iv) Iweke mikakati ya kuiwezesha Bodi ya Utalii Tanzania kuwa huru, kujiendesha na kujitegemea kimapato ikiwa ni pamoja na kufanya uwekezaji na kuongeza vyanzo vya mapato; na

(v) Iongeze nguvu ya utangazaji wa Utalii kwenye masoko ya kimkakati ili kuendelea kuongeza idadi ya watalii nchini.

**F. Tozo za Maendeleo ya Utalii (TDL)**

Kamati inashauri Serikali kutafakari upya malengo, mgawanyo na usimamizi wa fedha hizi ili tija iliyokusudiwa ipatikane.

**G. Migogoro ya Mipaka na Utwaaji wa Ardhi**

Kamati inashauri kuwa, Serikali: -

(i) Iendelee kutatua migogoro ya mipaka nchini kati ya Wananchi na Hifadhi; na

(ii) Ihakikishe inapotwaa maeneo kwa ajili ya uhifadhi pamoja na shughuli zingine za maendeleo, wananchi wanalipwa fidia stahiki na kwa wakati kama Katiba na Sheria za Ardhi zinavyoelekeza.

**H. Mashindano ya Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON 2027)**

Kamati inashauri kuwa, Serikali ihakikishe inaweka mikakati ya kutumia vizuri fursa ya uwepo wa mashindano haya ili kutangaza vivutio vya utalii nchini.

### 3.3 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika,** napenda kutumia fursa hii kwa niaba ya Kamati kukupongeza wewe binafsi, Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge, kwa namna ambavyo mmekuwa mkitimiza majukumu yenu kwa weledi mkubwa na hivyo kuliwezesha Bunge letu Tukufu kutimiza wajibu wake kwa ufanisi.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kutumia fursa hii pia kuwashukuru kwa dhati Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii, kwa ushirikiano waliouonesha katika kipindi chote cha Ziara za Ukaguzi wa Miradi na Uchambuzi wa Bajeti ya Wizara ya hii. Kutokana na ufinyu wa muda sitaweza kuwataja kwa majina, lakini naomba majina yao yaingizwe katika Kumbukumbu za Taarifa Rasmi za Bunge (*Hansard*). Majina ya Wajumbe hao ni haya yafuatayo:

1. Mhe. Timotheo Paul Mnzava, Mb - Mwenyekiti
2. Mhe. Mary Masanja, Mb - M/Mwenyekiti
3. Mhe. Festo R. Sanga, Mb - Mjumbe
4. Mhe. Haidary Hemed Sumry, Mb - Mjumbe
5. Mhe. Cosmas Mtesigwa Bulala, Mb - Mjumbe
6. Mhe. Fadhili Fabian Ngajilo, Mb - Mjumbe
7. Mhe. Silvery Luboja Salvatory, Mb - Mjumbe
8. Mhe. Yannick Ikayo Ndoinyo, Mb - Mjumbe
9. Mhe. Chiku Athuman Issa, Mb - Mjumbe
10. Mhe. Rashid Mohamed Mtima, Mb - Mjumbe

11. Mhe. Mgeni Hassan Juma, Mb - Mjumbe
12. Mhe.Selina Henry Kingalame, Mb - Mjumbe
13. Mhe. Mvita Mustafa Ali, Mb - Mjumbe
14. Mhe. Asia Abdulkarimu Halamga, Mb - Mjumbe
15. Mhe. Taska Restituta Mbogo, Mb - Mjumbe
16. Mhe. Khamis Ali Vuai, Mb - Mjumbe
17. Mhe. Hadija Shabani Taya, Mb - Mjumbe
18. Mhe. Joshua Samweli Nassari, Mb - Mjumbe
19. Mhe. Issa Ally Mchungahela, Mb - Mjumbe
20. Mhe. Amina Good said, Mb - Mjumbe
21. Mhe. Rose Cyprian Tweve, Mb - Mjumbe
22. Mhe. Juliana Daniel Shonza, Mb - Mjumbe

**Mheshimiwa Spika,** kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati, napenda kutumia fursa hii kuwashukuru Waziri wa Maliasili na Utalii, Mhe. Dkt. Ashatu Kachwamba Kijaji (Mb) na Naibu Waziri, Mhe. Hamad Hassan Chande (Mb) kwa ushirikiano wao mkubwa ambao umechangia kuiwezesha Kamati kutekeleza shughuli zake kwa ufanisi katika sekta hii. Aidha, nawashukuru pia Watendaji wote wa Wizara ya Maliasili na Utalii chini ya uongozi wa Katibu Mkuu, Dkt. Hassan Abbasi, kwa ushirikiano na mchango wao katika kipindi chote cha utekelezaji wa majukumu ya kikanuni ya Kamati.

**Mheshimiwa Spika,** mwisho lakini si kwa umuhimu, kwa namna ya pekee, nawashukuru Watumishi wa Bunge wakiongozwa na Katibu wa Bunge, Ndg. Baraka I. Leonard, kwa kuongoza vyema uratibu

wa shughuli za Kamati na Bunge kwa ujumla hadi kukamilika kwa Taarifa hii na kuwasilishwa mbele ya Bunge lako Tukufu.

**Mheshimiwa Spika,** Baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu, lipokee na kuijadili Taarifa hii pamoja na Taarifa ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maliasili na Utalii **(Fungu 69),** kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja.

**Mheshimiwa Spika,** Naomba kuwasilisha.

Timotheo Paul Mnzava, Mb
**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ARDHI, MALIASILI NA UTALII**

15 Mei, 2026